**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**





**HATI YA MAUZO YA SHAMBA/KIWANJA KILICHOPO MTAA WA KIJAKA KATA YA KIMBIJI**

**SEHEMU YA KWANZA:Kiapo cha manunuzi**

Mimi Ndg/Bi…OBEID MBAHI MWANGWA…Nikiwa na akili zangu timamu na bila kushawishiwa na mtu yeyote, leo tarehe…08/03/2021…nimeamua kumuuzia shamba/kiwanja/viwanja Ndg…PHOSE FOR AFRICA LIMITED… kilichopo/vilivyopo mtaa wa kijaka,Na… – … kitalu… – …Kwa thamani ya shilingi…24,000,000 (Heka tano (5)) (Kwa maneno…SHILINGI MILIONI ISHIRINI NA NNE TASHMU…)

**SEHEMU YA PILI:Mipaka ya kuzunguka eneo husika(Mfano:Barabara,taasisi,majirani n.k)**

**.Mashariki**…ZACKIEM - BARABARA…

**.Magharibi**…OBEID MWANGWA…

**.Kaskazini**…BARABARA - (MPEMBA)…

**.Kusini**…ALLY BARAKA…

**SEHEMU YA TATU:Ukiri/Uthibitisho wa wahusika na mashaidi zao kushiriki mauziano**

| JINA | UHUSIKA WAKE | SAHIHI |
|---|---|---|
| OBEID MBAHI MWANGWA | Muuzaji | |
| PHOSE FOR AFRICA LIMITED | Mnunuzi | |
| LISSA OBEID MWANGWA | Shahidi wa Muuzaji | |
| SEBASTIONI GASPEL SYALO | Shahidi wa Mnunuzi | |

**SEHEMU YA NNE:Uthibitisho wa kiongozi serikali ya mtaa kusimamia mauzo**

| JINA | SAHIHI/MUHULI | CHEO/NAFASI | TAREHE |
|---|---|---|---|
| GWANTWA G. MWAKABULI | | MEO | 08/03/2021 |

# MKATABA WA MAUZO ENEO

**KATI YA**

**OBEID MBAHI MWANGWA NA GRACE OBEID MWANGWA**
**(WAUZAJI)**

**NA**

**PHOSE FOR AFRICA LIMITED**
**(MNUNUZI)**

---

**KWA MAUZO YA ENEO LILILOPO KATA YA KIMBIJI MANISPAA YA KIGAMBONI.**

---

# MKATABA WA MAUZO YA ENEO

**Mkataba huu umesainiwa leo hii Manispaa ya Kigamboni Tarehe 05/03, 2021.**

**KATI YA**

**OBEID MBAHI MWANGWA na GRACE OBEID MWANGWA wa Dar Es Salaam** ambao katika Mkataba huu wataitwa "wauzaji", (ambao utawahusisha warithi wake, wawakilishi, ndugu na jamaa zake) kwa Upande Mmoja wa Mkataba;

**NA**

**PHOSE FOR AFRICA LIMITED** wa Sanduku la Posta **76636 Dar Es Salaam**, ambaye katika Mkataba huu ataitwa "Mnunuzi", (ambalo utahusisha warithi wake, wawakilishi, ndugu na jamaa zake) kwa Upande wa Pili wa Mkataba.

**KWA KUWA** Wauzaji ni wamiliki halali wa eneo na maendelezo yote yaliyopo katika **eneo hilo** ndani ya Manispaa ya Kigamboni ambalo katika Mkataba huu litaitwa "Eneo" ambalo mipaka yake yote imeonyeshwa na kutambulishwa kwa Mnunuzi mbele ya mashahidi wote waliotia sahihi zao hapa chini.

**NA KWA KUWA** wauzaji wameamua kumuuzia Mnunuzi eneo hilo pamoja na vyote vilivyomo katika eneo hilo, kwa mujibu wa masharti yaliyopo katika Mkataba huu na kwamba Mnunuzi ameshakagua na kutembelea eneo hilo na kuridhika na hali iliyopo katika eneo hilo **lenye ukubwa heka tano (5).**

**HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDA KAMA IFUATAVYO:**

**Kwamba,** Wauzaji watauza na Mnunuzi atanunua eneo hilo **lenye ukubwa wa heka tano (5)** likiwa halina Mgogoro au Migogoro yoyote ile kutoka kwa ndugu wa wauzaji wala mtu yeyote yule kwa **Shilingi za Kitanzania Milioni ishirini na nne tu (24,000,000/=) na kwa kila heka ni milioni 4,800,000=** Kwa kusaini Mkataba huu wauzaji wanakiri kupokea kiasi hicho cha fedha na anatamka wazi kuwa hana madai yoyote yale dhidi ya Mnunuzi kwa mauzo ya eneoa hilo.

1. **Kwamba,** mipaka ya eneo ni kama ifuatavyo;-

   a) Kaskazini –

   b) Kusini –

   c) Mashariki –

   d) Magharibi –

2. **Kwamba,** Pande zote mbili katika Mkataba huu zinakubaliana kwamba wauzaji watamkabidhi Mnunuzi nyaraka zote zinazohusiana na umiliki wa eneo hilo pamoja na barua za mawasiliano zozote alizofanya kwa maandishi mbalimbali kuhusiana na ufuatiliaji wa umiliki wa eneo hilo.

3. **Kwamba,** Mkataba huu unashuhudia kwamba wauzaji watamtambulisha Mnunuzi kwa serikali za mitaa ambapo eneo hilo lipo ikiwa ni pamoja na Mtendaji wa kata ili kuepuka usumbufu baadae.

4. **Kwamba,** pande zote mbili za Mkataba huu zitaendelea na taratibu zote za kisheria za kuhamisha miliki ya eneo hilo toka kwa wauzaji kwenda kwa Mnunuzi.

5. **Kwamba,** wauzaji wanamhakikishia Mnunuzi kwamba atakaa katika eneo hilo huru na hatobughudhiwa na mtu yeyote yule na kwamba ameshalipa madeni yote yanayohusu eneo hilo ikiwa ni malipo ya Manispaa, na kwamba hakuna deni lolote atakalolikuta Mnunuzi katika eneo hilo lililoachwa na wauzaji.

6. **Kwamba** yeye ni Mmiliki halali wa eneo hilo na pia endapo Mnunuzi atapoteza umiliki wa eneo hilo kutokana na wauzaji kutokuwa na umiliki halali na thabiti basi WAUZAJI watawajibika kumfidia MNUNUZI fedha za ufuatiliaji na usumbufu wowote utakaojitokeza.

**KWA USHUHUDA** pande zote mbili katika Mkataba huu zimesaini Mkataba huu siku na tarehe inayoonekana hapa chini:




IMESAINIWA NA KUTOLEWA DAR ES SALAAM na **OBEID MBAHI MWANGWA na GRACE OBEID MWANGWA** ambaye ninamfahamu/ametambulishwa kwangu na…………………………………………… ninayemtambua leo hii tarehe ……05…… Mwezi ……03…, 2021.

……………………
**WAUUZAJI**

**Shahidi:** Jina:- LISSA OBEID MWANGWA

Saini: ……………………

Tarehe: - 05/03/2021

**Mbele yangu:-**

Jina:- Saida Iddy Mshana

Saini: ……………………

Tarehe: - 05/03/2021

Wadhifa: **WAKILI**

IMESAINIWA NA KUTOLEWA Dar Es Salaam na **PHOSE FOR AFRICA LIMITED** ambaye ninamfahamu/ametambulishwa kwangu na……………………………… ninayemtambua leo hii tarehe 05 Mwezi ..03, 2021

……………………
**MNUNUZI**
MENEJA WA KAMPUNI

**Shahidi:** Jina: - SEBASTIAN GASPER SYALO

Sahihi: ……………………

Tarehe: - 05-03-2021

**Mbele yangu:-**

Jina:- Saida Iddy Mshana

Saini: ……………………

Tarehe: - 05/03/2021

Wadhifa: **WAKILI**